JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

MAHAKAMA

KATIKA MAHAKAMA YA MWANZO LUSHOTO

DOCHI

SHAURILA MADAI NA 4/2017

YUSUMA

AUTOSPARE&GARAGE……..

..MDAI (SM1)

DHIDI YA:

MKURUGENZI MTENDAJI WA HALMASHAURI YAWILAYA YA LUSHOTO……MDAIWA (SU1)

MBELE YA R.V.KASWAGA- HAKIMU MKAZI

WASHAURI: **1. Zuberi Guga**

2. Zaujia Lubwaza

AMRI YA MWISHO: 6/4/2017

TAREHE YA HUKUMU: 24/4/2017

HUKUMU

Katika hukumu hii, mdaiwa (SU1), Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya Lushoto anadaiwa shilingi milioni kumi na sita laki saba, tisini na nne elfu na mia sita na Arobaini (Tsh. 16,794, 640/=) na Yusuma Autospare Garage.

Maelezo katika hati ya madai ya tarehe 3/3/2017 ambayo ipo ndani ya jalada la kesi yanaeleza kuwa Yusuma Autospare & Garage anamdai Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Lushoto madai ya fedha Tsh. 16,794,640/= ambayo walimtengenezea vifaa vya ofisini kwao ambavyo ni magari,

pikipiki, na kumuuzia vipuri vyenye jumla ya thamani iliyotajwa hapo juu. Kazi hiyo walifanya tangu 2011 hadi 2015 cha ajabu mpaka sasa amekaidi kulipa fedha hizo.

Mahakama hii ilipofungua jalada la shauri hili, ilitoa amri ya wito kwa SU1 mnamo tarehe 9/3/2017 ili afike tarehe 15/3/2017 na tarehe hiyo SU1 hakuja mahakamani licha ya kusainiwa kwa hati hiyo na ofisi ya SU1 na kugongwa muhuri wa Halmashauri ya Wilaya Lushoto.

Hata kabla ya tarehe 9/3/2017, mnamo tarehe 1/3/2017 mahakama ilitoa pia kuitwa shaurini ili SU1 afike tarehe 3/3/2017 ili asomewe dai la SM1, lakini hata tarehe hiyo 3/3/2017 pia hakufika, licha ya sahihi na muhuri wa ofisi ya SU1 kuwepo katika hati ya wito.

Hii ilifanya mahakama hii kusikiliza shauri hili upande wa SM1 pekee kwa kuona kuwa SU1 anayo taarifa ya shauri hili na hataki kufika mahakamani.

SM1 alidai kuwa na mashahidi wanne japo siku ya kusikilizwa kwa shauri hili SM1 alidai kuwa na shahidi mmoja tu.

Araphat Abubakari Mzeekwa niaba ya Yusuma Auto Spare &Garage, kwa kiapo, mnamo 27/3/2017 alieleza mahakama hii kwamba anamfahamu SU1 kama Halmashauri kupitia kwa DED ambaye aliwapa kazi ya kutengeneza vifaa vya mitambo, magari na pikipiki tangu 2011.

Tangu wakati huo, SU1 anadai wamekuwa wakitengenezewa magari, pikipiki na kuchukua vipuri pamoja na kutengenezewa magari hayo na kuwekewa vipuri vyenyewe kwa matengenezo na kwamba matengenezo yakikamilika analipa gharama zote.

Licha ya kupatiwa huduma na vipuri, SU1 alisitisha malipo.

Imeelezwa na**Araphat Bakari Mzee** kwamba huduma ya matengenezo inapotimia basi huwa wanajaza" Local Purchase Order" (LPO) ambapo SU1 anatakiwa alipe kwa kutumia LPO hiyo.

Kabla ya 2016, SU1 amekuwa akikumbushwa malipo kwa mdomo lakini kuanzia 2016 amekuwa akikumbushiwa kwa maandishi, ingawa hajajibu hata mara moja, japo kwa mdomo amekuwa akiahidi kulipa lakini hajafanya hivyo.

Nyaraka ambazo zimepokelewa baada ya kutolewa na ndugu **Araphat Abukakari Mzee** ni kama ifuatavyo na maelezo yake;

1. **Exh. P-1**, ambayo nikaratasi la Yusuma Auto Spare & Garage ambayo ni ya tarehe 17/10/2017 ikiwa ni kusudio la kuleta kesi mahakamani ikienda kwa DED wa Lushoto District Council.
2. **Exh. D-2,** Delivery Notes za tarehe 29/9/2011, 5/1/2012, 19/7/2012, 25/1/2013, 27/1/2013, ambazo zilikuwa zinasainiwa na madereva wa Halmashauri.
3. **Exh. P-3**, Orodha ya Local Purchase Orderszilizorudishwa na SU1 ya tarehe 13/9/2011 – 25/6/2013.
4. **Exh. P- 4**, orodha ya namba za LPO ya tarehe 19/5/2016 ambazo SM1 amedai hazikurudi.

5. **Exh. D-5**, Dispatch book iliyosainiwa tarehe 19/5/2016 kwa kupokea Invoice toka Yusuma Auto Spare &Garage.
6. **Exh P- 6** Bank Statement ya Yusuma Auto Spare& Garage ya tarehe 3/1/2017 ya benki ya NMB.
7. **Exh D-7**, Local Purchases Orders (kwa pamoja).
8. **Exh. P-8,** Dispatch book ya tarehe 17/10/2016, iliyosainiwana ofisi ya DED – Lushoto ikiwa ni nia ya kushitaki.

Kuhusu **Exh P-6**, **Araphat Mzee** amedai kuwa ni kuthibitisha kuwa malipo hayo hayawahi kuingizwa tangu 2011 hadi 2017.

Akihojiwa na mahakama hii, **Araphat A. Mzee** amedai kuwa hajatenga kwa mwaka walikuwa wanadai kiasi gani na kuwa kwenye deni hilo SU1 hajalipa kiasi chochote.

Imedaiwa kwamba biashara hii ni ya Jumuiya na yeye Araphat A. Mzee amedai anasimamia kwa niaba ya Yusuma Auto Spare &Garage na kwamba vifaa vilipokuwa vinapelekwa hapo ofisini alikuwa anakutwa mtu yoyote dukani na LPO ndio inaeleza nini kinatakiwa kutengenezwa.

Imedaiwa pia kwamba suala hili limeshawahi kufanyiwa usuluhisho mahakama ya Wilaya mara tatu na hakuna aliyekwenda zaidi ya mara moja tu kwenda mtu akisema mwanasheria hayupo na kuwa SU1 amekuwa akidai kuwa watalipa wanavyotaka na kwamba serikali haiwezi kushikiliwa vitu vyake kwani serikali haiishi madeni.

Kutokana na madeni hayo, inadaiwa wateja wa Yusuma wanakosa uaminifu pamoja na mafundi na hivyo wanashindwa kuendelea na biashara na hivyo kutishia kufilisika kwani wao pia wanadaiwa.

SM2, **Paulo Juma Mtoi**, yeye amekuwa fundi wa Yusuma Auto Spare& Garage na kwamba yeye anatengeneza pikipiki inapoletwa na Halmashauri ikimlipa Yusuma Auto Spare& Garage basi ndipo yeye analipwa. Matokeo yake, anadai SM2 wamekuwa wakisubiri na hatimaye hatua ikawa ni kuleta kesi mahakamani.

Akihojiwa, SM2 amedai amekuwa akitengeneza pikipiki za Halmashauri tangu 2011- 2015, wakati vipuri vikitoka Yusuma Auto Spare& Garage. SM2 anadai yeye hajalipwa kwani SU1 hakumlipa tajiri yake na kwa sasa SM2 anadai amesimama kazi kwa muda kwani hajapewa pesa na kwa gharama za kutengeneza pikipiki moja kwa mwaka ilikuwa kati ya Tsh. 15,000/= na Tsh. 70,000/= na kwamba hajui kwa zote maana zinakuja nyingi, na kuwa kwa sasa amesimama kufanya kazi.

SM2 amedai hajui gharama za utengenezaji wa magari na kuwa yeye yupo peke yake uwanjani, na kuwa SM1 ana biashara ya duka la spea pamoja na kutoa ‘service’.

SM2 anadai kuwa kabla ya kazi alisema ni ya halmashauri na kwa kuwa sio kazi ya papo kwa papo, SM2 aliambiwa tajiri akilipwa naye atalipwa.

Huo ndio ukawa mwisho wa ushahidi upande wa madai na ndipo baada ya kufunga ushahidi huo, mahakama ilipanga tarehe ya hukumu.

Baada ya kusikiliza shauri upande wa madai tumejiuliza swali moja,

Je SU1 anapaswa kulipa shilingi 16,794,640/= kama alivyodaiwa katika kesi hii?

Wajibu katika kesi za madai kuthibitisha kwamba anayepaswa kulipa deni au kutekeleza wajibu uliodaiwa, upo upande wa mdai kwa mujibu wa kanuni ya 6 ya Tangazo la Serikali Na. 22/1964 ambalo ni Kanuni za Ushahidi katika Mahakama za Mwanzo.

Maoni ya **Zuberi Guga, Zaujia Lubwaza na Kaswaga.R.V. (HakimuMkazi)**kwa pamoja:-

Baada ya mahakama hii kupima vielelezo vilivyotolewa yaani Exh.D-1 mpaka Exh. D- 8 pamoja na ushahidi wa **Araphat Abubakari Mzee** kwa niaba ya Yusuma Auto Spare & Garage na **Paulo Juma Mtoi** tumeona kuwa SU1 hapaswi kulipa pesa hizo, Tsh. 16,794,640/= kwa kuwa pamekuwepo na matatizoyakisheria katika kesi hii.

Mahakama imeshindwa kujua hasa nafasi ya Araphat Abubakari Mzee katika Yusuma Auto Spare & Garage na kujiuliza imekuwaje tena aje afungue kesi hapa mahakamani.

Katika ushahidi, ameeleza yeye ameshitaki kwa niaba ya wenzake katika jumuiya lakini hajaleta shahidi yoyote ambaye anathibitisha kwamba kama sehemu ya jumuiya wamemtuma Araphat (supra) kuja kufungua madai haya kwa niaba yao.

Tumeshindwa kujua pia ikiwa Yusuma Auto Spare & Garage nikampuni au shirika lisilo kampuni (yaanipartnership /Firm inayoanzishwa kwa kuruhusiwa na Sheria ya Mikataba Sura ya 345 R.E 2002). Ikiwa basi Yusuma (supra) nipartnership bila shaka haikutakiwa kufungua kesi (kushitaki kwa jina lake *"cannot sue in its own name"* kama ilivyo katika kesi hii. Japo katika mazingira fulani ya upekee pia *"partnership"* inaweza kushitaki kwa jina lake, lakini bado idadi na majina ya washirika wa jumuiya hiyo ilipaswa kujulikana hapa mahakamani.

Badala yake ilitakiwa angalau mmojawapo wa wanajumuiya *"partner"* au wana jumuiya wote au kadhaa "*partners"*waje / aje kufungua kesi hii kwa niaba ya wenzake na wengine waje washuhudie uwepo wa mikataba miwili;kwanza juu ya uwepo wa jumuiya [kama ni wa mdomo au maandishi], na pili, mkataba wao na SU1.

Endapo pia jumuiya *(partnership)* hiyo ingekuwa imesajiliwa kwa mujibu wa **Business Names (Registration) Act, Sura ya 213, R.E 2002** pamoja na kufanya kazi kwa mujibu wa **Business Activities Registration Act, 2007**, **Law of Contract Act** (supra),**Registration of Documents Act, CAP 117 R.E 2002**, basi illitakiwa upande wa madai ulete**"Partnership Deed"**

kuthibitisha uwepo wa jumuiya hiyo. Hili halipo pia katika shauri hili maana nyaraka hiyo ingetusaidia kujua uwepo wa*partnership* hiyo.

Kama Yusuma Auto Spare & Garage ingekuwa ni kampuni iliyoanzishwa kwa mujibu wa **Companies Act CAP 212 R.E 2002**, bila shaka ingekuwa ni sahihi kufungua kesi kwa jina lake kwani kampuni ni mtu kama ilivyoelezwa katika kesi ya*Salomon V Salomon& Co. LTD [1987] AC 22*.

Upande wa madai umeshindwa kulithibitsha hili pia na hivyo kuacha wasiwasi kwamba aliyekuja mahakamani kufungua kesi na kutoa ushahidi anayo nguvu kisheria ya kufanya hivyo. Kwa mujibu wa ushahidi wa SM2 pia hatujaona unatosha kuthibitisha ni kwanini SU1 alipepesa tajwa hapo juu kwani yeye ni muajiriwa tu ambaye hata madai dhidi ya SU1 hayafahamu sawasawa kwa kupima ushahidi wake.

Hata majina ya watu wanaohusika na Yusuma Auto Spare & Garage hayajaelezwa na upande wa madai hivyo inakuwa vigumu mahakama kutoa amri kuhusu fedha hizo kulipwa pasipo kujua zinaenda kwa nani na nani hasa ukizingatia**Araphat Abubakari** amedai tu kwamba yeye anashitaki kwa niaba ya wenzake wakati hati ya madai aliyojaza inaonyesha kwamba,*"Mimi Yusuma Auto Spare & Garage ninamdai Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Lushoto …."*

Hii pia ina maana Yusuma Auto Spare & Garage imepewa sifa ya mtu (mdai) na ilihali uthibitisho wa uwepo wake haujatolewa mahakamani kama tulivyoeleza hapo juu.

Hivyo tumeona madai hayajathibitika, kwa mujibu w*akifungu cha 3 (i) cha Nyongeza ya IV Sheria ya Mahakama za Mahakimu Sura ya 11 Iliyorekebishwa Mwaka 2002.*

Washauri Sahihi ya: **ZuberiGuga**

Sahihi ya:**Zaujia Lubwaza**

Sahihi ya:**R.V.Kaswaga- Hakimu Mkazi**

24/4/2017

AMRI:-

Haki ya rufaa ipo wazi ndani ya siku thelathini (30) katika Mahakamaya Wilaya kwa ambaye hakuridhika na hukumu hii

Washauri Sahihi ya: **Zuberi Guga**

Sahihi ya:**Zaujia Lubwaza**

Sahihi ya:**R.V.Kaswaga- Hakimu Mkazi**

24/4/2017

Mahakama:- Hukumu hii imesomwa leo tarehe 24/4/2017 nami mbele ya washauri wawili, na Haruna Yusuph ambaye ni rafiki wa **Araphat Abubakari Mzee** ambaye amemtuma kumsikilizia hukumu hii.

Sahihi ya:**R.V.Kaswaga- Hakimu Mkazi**

24/4/2017